**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM**

**MAOMBI YA MAREJEO NA. 892 YA 2019**

**BAINA YA**

**PEACOCK HOTEL LTD..................................... MLETA MAOMBI**

**NA**

**VERONICA NDUMBARO...................................MJIBU MAOMBI**

**UAMUZI**

*Tarehe ya Amri ya mwisho: 23/06/2021*
*Tarehe ya Uamuzi: 05/07/2021*

**A. Msafiri, J.**

Msingi wa maombi haya ni kwamba mnamo tarehe 14/03/2018 Veronica Ndumbaro aliyekuwa mwajiriwa wa Peacock Hotel Ltd (sasa mjibu maombi) alifungua mgogoro wa kazi mbele ya Tume akipinga kuachishwa kazi na mwajiri wake isivyo halali. Aliomba Tume imuamuru mwajiri kumlipa yeye mwajiriwa mafao yatokanayo na kuachishwa kazi.

Wakati wa kusikiliza shauri hili, Mwajiri (sasa mleta maombi) hakufika mbele ya Tume kwa ajili ya usuluhishi tarehe 24/04/2018, na tarehe 07/06/2018. Kwa kutumia kifungu cha 87(3)(b) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura 366, Msuluhishi aliamua kusikiliza shauri hilo kwa upande mmoja. Baada ya usikiizwaji, Uamuzi ulitolewa tarehe 22/02/2019 ambao ulimpa Tuzo Mwajiriwa.

Baada ya kupata taarifa za Tuzo iliyotolewa kwa mwajiriwa ambapo Tume iliamuru kuwa Mwajiri amlipe Mwajiriwa jumla ya shilingi za kitanzania 5,261,538/48 pamoja na cheti cha Utumishi. Mwajiri alipata nakala ya Tuzo hiyo tarehe hiyohiyo 22/02/2019 na kutoridhishwa na Uamuzi huo hivyo alifungua maombi madogo ya marejeo mbele ya Tume akiomba kutengua Uamuzi wa Tuzo hiyo ya upande mmoja. Maombi hayo yaliwasilishwa Tume na kusikilizwa tarehe 06/08/2019, na Uamuzi kutolewa tarehe 15/10/2019.

Katika maombi hayo, sababu kuu iliyotolewa na Mwajiri ni kwamba hakupewa hati za taarifa ili kufika mbele ya Tume na kujitetea kwa mujibu wa Sheria, na kwamba Mwajiriwa alikuwa na nafasi nzuri ya kufikisha hati za taarifa kwa Mkurugenzi (Mwajiri) lakini hakufanya hivyo. Mwajiri alieleza Tume kuwa pia hakupewa Fomu Na 1 ya maombi kama inavyotakiwa kisheria.

Hata hivyo, Tume ilijiridhisha kuwa Mwajiri alipewa hati za wito mara mbili yaani Hati ilitolewa tarehe 14/03/2018 na ilitolewa tarehe 27/04/2018 na kuwa hati hizo zilipokelewa na kugongwa muhuri wa Mwajiri. Kwa msingi huo, Tume ilitupilia mbali (dismiss) maombi hayo. Uamuzi huo ulitolewa tarehe 15/10/2019. Mwajiri hakuridhika na uamuzi

Labour Court Tz

huo na amewasilisha maombi mbele ya Mahakama hii akitoa sababu zifuatazo;

i) *Kwamba Msuluhishi alikosea kwa kushindwa kukubali maombi ya kutengua Uamuzi wa upande mmoja kwani hati ya wito haikutolewa kwa mwombaji kama inavyotakiwa kisheria.*

ii) *Kwamba Msuluhishi alikosea kwa kuamua kuwa mleta maombi (applicant) alikuwa amepokea Hati ya wito kutoka kwa Mjibu maombi (respondent) kupitia kwa "Operation Manager" kwani Kampuni ya mleta maombi haina nafasi ya Operation Manager.*

iii) *Kwamba Msuluhishi alikosea kwa kushindwa kutengua amri ya upande mmoja kwani kulikuwa na masuala ya kisheria ya kujadiliwa (determined on merit) endapo shauri hili lingesikilizwa kwa pande zote.*

Wakati wa usikilizwaji wa maombi haya mbele ya Mahakama, pande zote mbili zilikuwa zinawakilishwa. Mleta maombi aliwakilishwa na Richard Mwalingo, Wakili na mjibu maombi aliwakilishwa na Denis Mwamkwala, Mwakilishi binafsi. Aklifanya mawasilisho ya msingi kuunga mkono maombi haya, Wakili wa Mleta maombi alijieleza kwenye hoja za kisheria kama zilivyoorodheshwa kwenye hati ya kiapo ya Deostalit Protas ambae



Labour Court TZ.

ni Principal Officer wa Mleta maombi, kipengele cha 5. Alieleza kuwa kuhusu hoja namba 5.1, ambapo Msuluhishi alisema kuwa hakukuwa na sababu ya msingi ya kutengua Uamuzi wa upande mmoja, Mleta maombi anaona kuwa anayo sababu ya msingi kwani shauri (mgogoro) wa kazi ulifunguliwa nje ya muda kinyume na Kanuni ya 10(1) ya G.N. 64 ya 2007 ambayo inaeleza kuwa mtu ambae hakuridhika na maamuzi ya mwajiri afungue shauri ndani ya siku 30.

Wakili alieleza kuwa katika shauri mbele ya Tume, Mjibu maombi anaonyesha alifukuzwa kazi tarehe 13/10/2016, lakini katika Fomu Na 1, Mjibu maombi anaonekana kufungua shauri mwaka 2018, na kwa msingi huo shauri hilo lilifunguliwa mbele ya Tume nje ya muda bila kupata ruhusa ya Tume. Kwamba tarehe 07/10/2018, muamuzi alifuta shauri hilo kwa kutotokea mbele ya Tume kwa mlalamikaji. Tarehe 01/02/2019, shauri hili lilirejeshwa tena mbele ya Tume bila mlalamikaji kuomba kutengua Uamuzi wa awali wa kutupilia shauri hilo kwa non-appearance.

Endapo hili lingefanyika, ingempa mjibu maombi (sasa mleta maombi) nafasi ya kuitwa shaurini kusikilizwa hoja zake. Tarehe 01/02/2019 shauri lilisikilizwa mbele ya Tume kwa upande mmoja bila kuwepo mlalamikiwa ambapo mlalamikiwa hakupewa wito wa kuitwa shaurini.

Wakili Mwalingo alirejea Kanuni ya 28(4) ya G.N. 64 ya 2007 ambayo inataka endapo shauri limetupiliwa mbali, Tume itoe nakala ya Uamuzi huo kwa pande zote mbili. Wakili alieleza kuwa Mleta maombi hakuwa na taarifa mpaka alipopata taarifa kuhusu Tuzo ya upande mmoja. Katika hoja za kisheria namba 5.2 na 5.3, Wakili alieleza kuwa Msuluhishi alijiridhisha kuwa hati za wito zilitolewa kwa Daniel Mfugale ambae alitambuliwa kama Operational Manager wa Peacock Hotel, hata hivyo hati hizo hazikuwa na Muhuri wa Kampuni na zilitolewa kinyume na Kanuni 6 na 7 za G.N. 64 ya 2007.

Katika hoja na 5.4, Wakili alieleza Mahakama kuwa katika kufanya maamuzi yake, Msuluhishi alitumia vifungu vya Civil Procedure Code, Order IX Rule 13(1). Kwamba Msuluhishi hakutakiwa kutumia vifungu hivi kwani mashauri ya kazi yanayoendeshwa na Tume yana sheria zake zinazojitosheleza kuyaendesha. Alirejea kesi ya **Barclays Bank vs. Chiza Shungu,** Revision No 42 ya 2015 Labour Court Digest Vol1, ambapo ilielezwa kuwa sheria ya mwenendo wa mashauri ya madai itatumika katika mashauri ya kazi endapo tu kuna ombwe (lacuna).

Akirejea katika kesi iliyopo mbele ya Mahakama, Wakili alieleza kuwa hakukuwa na ombwe kwani kifungu cha 87(5) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, na Kanuni za 6 na 7 za G.N. 64 ya 2007



Labour Court Tz.

zinajitosheleza katika kesi hii, na hivyo mwamuzi alikosea kuchukua mamlaka ya Mahakama kuu, Divisheni ya Kazi ambayo ndiyo yeye mamlaka ya kutumia sheria ya mwenendo wa mashauri ya madai pale ambapo kuna ombwe la kisheria. Wakili wa mleta maombi alisisitiza mbele ya Mahakama kuwa shauri mbele ya Tume lilikuwa na mapungufu ya kisheria kama yanavyobainishwa kwenye hoja na 5.5, 5.6 na 5.7 kwenye Hati ya kiapo, hivyo endapo Mleta maombi angepata nafasi ya kusikilizwa angeweza kuiongoza Tume kuhusu mapungufu yote ya kisheria yaliyojitokeza ili Tume iweze kufikia Uamuzi sahihi na wa haki. Alisisitiza kuwa kitendo cha kunyimwa haki ya kusikilizwa ni kinyume na Ibara ya 13(6)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Alihitimisha kwa kuomba kuwa yaliyomo kwenye kiapo cha mleta maombi yawe sehemu ya mawasilisho yake.

Akijibu mawasilisho ya mleta maombi, Mwakilishi binafsi wa mjibu maombi alieleza kuwa hakukuwa na sababu za msingi za Msuluhishi kusikiliza maombi ambayo yako nje ya muda. Vilevile, Mwakilishi alipinga hoja zilizotolewa na wakili wa mleta maombi kuwa maombi yaliyofunguliwa na Mwajiriwa yalikuwa nje ya muda. Alitoa ufafanuzi kuwa ni kweli barua ya kufukuzwa kazi aliyopewa Mwajiriwa (mjibu maombi) inaonyesha kuwa iliandaliwa tarehe 13/12/2016 lakini mjibu maombi

Labour Court Tz.

alipokea barua hiyo tarehe 28/2/2018 na akafungua mgogoro Tume tarehe 18/3/2018 ikiwa ni siku 18 tangu kupokea barua ya kufukuzwa kazi.

Mwakilishi alieleza kuwa ili kuthibitisha madai yake kuhusu tarehe ya kupokelewa barua ya kufukuzwa kazi, Mleta maombi angewasilisha attendance Register ili kuthibitisha kuwa Mjibu maombi aliondolewa kazini kwa tarehe 13/12/2016 na tangu wakati huo hakufika kazini. Kuhusu hoja ya kupokea hati ya wito, Mwakilishi alieleza kuwa, Mjibu maombi alifanya jitihada za kumpatia hati za wito Mleta maombi ili kuhudhuria katika hatua ya usuluhishi wa mgogoro lakini Mjibu maombi hakuweza kuhudhuria.

Alisisitiza kuwa ili kuficha ukweli kuwa hati hizo zilipokelewa nae, Mleta maombi hakuambatanisha hati hizo kwenye maombi yake mbele ya Mahakama hii, na kwa kuwa hii ni hoja ya msingi, hati hizo zingeambatanishwa ili kusaidia Mahakama kubaini ukweli. Alirejea kesi ya **Edward Bachwa & 3 Others vs. Attorney General & Another,** Civil Application No. 128 of 2006 (unreported) ambapo ilielezwa kuwa sio kazi ya Mahakama kutafuta document ambayo Mwombaji anabishania. Alisisitiza kuwa shauri lilifunguliwa ndani ya muda mbele ya Tume na kwa mamlaka iliyonayo chini ya kifungu 87(3)(b) cha Sheria ya Ajira na

Labour Court Tz.

Mahusiano kazini, Tume ilisikiliza upande mmoja na kutoa Tuzo kwa Mjibu maombi.

Hivyo, aliiomba Mahakama kuwa maombi haya yatupiliwe mbali kwani hayana msingi wowote. Aliomba kujumuisha hoja zilizomo kwenye kiapo kinzani cha Mjibu maombi kuwa sehemu ya mawasilisho yake upande wa mjibu maombi. Akifanya mawasilisho ya nyongeza (rejoinder submission), Wakili wa Mleta maombi alirudia mawasilisho yake ya msingi. Pia aliongezea kuwa hati za wito ziliwasilishwa na mtu asie halali kisheria, kwani kwa mujibu wa Sheria, hati za wito zinatakiwa kuwasilishwa na "process server" anayetambulika kisheria. Pia aliomba Mahakama kutozingatia kesi iliyorejewa na Mjibu maombi ya **Edward Bachwa vs. Attorney General** (supra) kwani inazungumzia suala tofauti na lililopo mbele ya Mahakama.

Baada ya kupitia hoja za pande zote mbili pamoja na hati ya kiapo na kiapo kinzani, nimebaini kuwa pande zote mbili ziliwasilisha hoja zaidi ambazo zinaenda kwenye msingi wa shauri lililoamuliwa mbele ya Tume ambayo ilimpa Tuzo Mjibu maombi ya upande mmoja, badala ya kujikita kwenye Uamuzi wa Tume wa kutupilia mbali maombi ya kutengua Uamuzi wa upande mmoja.

Maombi yaliyowasilishwa mbele yangu ni ya kupinga Uamuzi mdogo wa Tume wa tarehe 15/10/2019 wa kutupilia mbali (dismissal) maombi ya kutengua Uamuzi wa upande mmoja. Hata hivyo hoja za pande zote mbili zilienda pia kwenye kupinga uamuzi wa tarehe 22/2/2019 ambao ulimpa Tuzo Mjibu maombi. Hivyo katika uchambuzi wa hoja na ushahidi, Mahakama itajikita katika hoja zinazopinga uamuzi wa tarehe 15/10/2019 ambao ndio msingi wa maombi haya.

Kwa minajili hiyo, Mahakama itajikita katika sababu Na. 4.1, 4.2, 4.3, na hoja za kisheria namba 5.1, 5.2, 5.3 na 5.4 katika hati kiapo ya Mleta maombi, na majibu yake katika hati kinzani ya Mjibu maombi na mawasilisho yao kuhusu hoja hizo. Kwa kuzingatia hilo Mahakama hii kwa ujumla wake inaona kuwa hoja za msingi kutolewa maamuzi ni kama zifuatazo;

*i)* *Endapo mleta maombi ametoa sababu za msingi za kutengua uamuzi wa upande mmoja.*

*ii)* *Iwapo Mleta maombi alipokea kikamilifu wito (properly served).*

*iii)* *Endapo Msuluhishi alikosea kisheria katika kufanya maamuzi yake na hivyo kufanya maamuzi hayo kuwa yametolewa kwa makosa.*

Kanuni ya 6 ya G.N. 64 ya 2007 inaeleza utaratibu wa uwasilishaji wa hati za wito baina ya pande mbili. Vilevile Kanuni ya 7 ya G.N. 64 ya 2007 inaeleza namna ya uthibitisho kuwa hati imepokelewa (proof of service of document).

Kwa kuanzia hoja ya pili kuhusu endapo hati za wito ziliwasilishwa na kupokelewa na Mjibu maombi, Mahakama ilipitia kumbukumbu za Tume ambapo katika uamuzi mdogo wa maombi ya kutengua uamuzi wa upande mmoja, Msuluhishi alijiridhisha kuwa hati mbili za wito zilitolewa na Tume ambapo hati ya kwanza ilitolewa tarehe 14/03/2018, hati inaonesha ilipokelewa na kugongwa muhuri na Bwana Daniel ambae ni Operational Manager wa mjibu maombi.

Tume ilitoa wito mwingine tarehe 27/04/2018, hati hiyo ilipokelewa na Bwana Daniel ambae ni Operational Manager wa Mjibu maombi na kugongwa muhuri lakini Mjibu maombi hakufika. Katika kumbukumbu zilizopo, ipo hati ya wito wa kusikiliza shauri tarehe 5 April 2018, ilichukuliwa na Veronica Ndumbaro (Mlalamikaji) ambae amesaini tarehe 21/03/2018 na hati hiyo kupokelewa na Daniel, Operational Manager, Peacock Hotel. Hati ina muhuri wa Peacock Hotel ambayo haina tarehe ya kupokea bali ina muda wa kupokelewa.

Labour Court TZ

Vilevile ipo hati ya wito wa usikilizwaji tarehe 04 Mei 2018, iliwasilishwa na Veronica Ndumbaro, Mlalamikaji tarehe 27/04/2018. Hati hiyo imepokelewa na Daniel, Operations Director Peacock Hotel, tarehe 27/04/2018.

Akitoa hoja zake, Wakili wa Mleta maombi alikanusha kuwa mleta maombi hakupokea hati za wito na hivyo hakuwa na taarifa za uwepo wa mgogoro huo mbele ya Tume. Aliieleza Mahakama kuwa Mwamuzi alikosea kujiridhisha kuwa hati zilipokelewa na Daniel Mfugale ambae alitambuliwa kama Operational Manager, hata hivyo hati hizo hazikuwa na mhuri (seal) ya kampuni na zilitolewa kinyume na Kanuni 6 na 7 za G.N. 64 ya 2007.

Kuhusu hoja hii na kwa kuzingatia kumbukumbu nilizoainisha, ninaona kuwa Mleta maombi hakukana kutomtambua Daniel Mfugale ila alieleza kuwa hati hazikuwa na seal ya Kampuni. Hata hivyo hati hizo zina muhuri wa Kampuni na hivyo Tume ilijiridhisha kuwa, Hati hizo zimepokelewa na Kampuni, Mahakama hii pia imeshindwa kubaini endapo Kampuni ya Mleta maombi ina "Seal" tofauti na muhuri unaoonekana kwenye hati ya wito wenye jina la Kampuni, anwani na mahali Kampuni ilipo. Hivyo, Mahakama inaona kuwa hati hizo zilipokelewa na mtu sahihi

Labour Court Tz.

ambae ni mmoja wa wafanyakazi wa Kampuni ya Mleta maombi na hivyo ni uthibitisho wa kupokea hati kwa Mleta maombi.

Kuhusu hoja ya kuwa hati ya wito ilitolewa na mtu ambae si sahihi na kwa mujibu wa Sheria inayotaka kuwa hati ya wito itolewe na "process server", wakili wa mleta maombi hakuieleza Mahakama ni Sheria ipi inayoweka takwa hilo kwani Kanuni ya 6(1) ya G.N. 64 ya 2007 inaeleza kuwa " *a party shall serve a document to other party".* Hivyo upande mmoja wa shauri ndio unahusika na kutoa hati na kuwasilisha kwa upande mwingine na kwa hili, hati ilitolewa na Veronica Ndumbaro ambae ni upande mmoja wa shauri.

Katika mawasilisho yake, Mleta maombi alieleza kuwa tarehe 07/10/2018 Mwamuzi alifuta shauri lililowasilishwa na Mlalamikaji. Katika mwenendo wa shauri mbele ya Tume, inaonyesha kuwa tarehe 07/10/2018 mgogoro ulifutwa kwa mlalamikaji aliewasilisha shauri (sasa mjibu maombi) kushindwa kufika mbele ya Tume. Hata hivyo, shauri hilo lilirejeshwa tena na kusikilizwa kwa upande mmoja tarehe 01/02/2019.

Kwa kuzingatia hoja zilizotolewa na wakili wa Mleta maombi, nimepitia kumbukumbu ili kuona endapo zipo hati za wito zilizotolewa kwa Mleta maombi kwa ajili ya usikilizwaji ulioanza baada ya Shauri kurejeshwa tena Tume mwaka 2019 baada ya kufutwa tarehe



Labour Court Tz.

07/10/2018. Hata hivyo nimebaini kuwa hati zilizopo ni zilizotolewa tarehe 27/04/2018 na 14/04/2018. Pia katika Uamuzi mdogo, Mwamuzi anaonekana kuchanganya miaka ya utolewaji wa hati hizo kwani anaeleza kuwa hati ya wito ya kwanza ilitolewa tarehe 14/03/2018 na pande kutakiwa kufika Tume tarehe 05/04/2019 kwa ajili ya usuluhishi hali ambayo isingewezekana hati ya wito kutolewa mwaka mmoja kabla ya usikilizwaji wa usuluhishi.

Vilevile, Msuluhishi katika ukurasa wa 4 wa uamuzi mdogo anaeleza kuwa hati ya pili ilitolewa tarehe 27/04/2018 na pande kuamuliwa wafike tarehe 04/05/2019. Mahakama inaamini kuwa makosa haya ni ya uandishi na Msuluhishi alikusudia mwaka 2018 na sio mwaka 2019. Pamoja na makosa hayo bado swali ni endapo hati za wito zilitolewa kwa Mleta maombi baada ya shauri hili kufutwa tarehe 07/10/2018 na kurejeshwa tena kwa utaratibu ambao haukubainishwa. Kwa kutobainishwa hili, Mahakama inakubaliana na hoja za Mleta maombi kuwa hakupata taarifa ya kurejeshwa shauri lililokuwa limefutwa na hakupata wito wa kusikiliza shauri hilo baada ya kurejeshwa.

Mahakama inakubali kuwa baada ya shauri hilo kufutwa tarehe 07/10/2018 na kurejeshwa tena tarehe 01/02/2019 na kuanza kusikilizwa, hakuna ushahidi unaoonyesha kuwa Mleta maombi aliitwa shaurini. Hivyo,

Labour Court Tz.

kwa uchambuzi huu, Mahakama inaona kuwa Mleta maombi alipokea kikamilifu hati za wito zilizotolewa Machi 2018 ya usikilizwaji wa 5 Aprili 2018, na iliyotolewa Aprili 2018 ya usikilizwaji wa 04 May 2018.

Mahakama inaona kuwa hakuna ushahidi wa wito uliotolewa kwa Mleta maombi baada ya shauri hilo kurejeshwa tena tarehe 01/02/2019 na kusikilizwa kwa upande mmoja. Hivyo Mahakama imejiridhisha kuwa Mleta maombi hakuwa na taarifa za kurejeshwa kwa shauri hilo na hivyo kutoweza kufika Tume na kusikilizwa na hii inajibu hoja kuwa Mjibu maombi hakupokea kikamilifu hati za wito na hii ilimnyima haki ya kusikilizwa.

Kuhusu hoja endapo Mwamuzi alikosea kisheria katika maamuzi yake, Mahakama imeona kuwa kuna makosa katika uamuzi mdogo kuhusu hati za wito zilizotolewa kwa mjibu maombi kama nilivyoeleza awali kuwa kuna mkanganyiko kati ya hati kutolewa mwaka 2018 au mwaka 2019. Vilevile, katika maamuzi yake, Msuluhishi hakubainisha kuwa shauri liliondolewa Tume tarehe 7/10/2018 baada ya mlalamikaji kutofika katika usuluhishi. Katika mwenendo wa shauri wa Tume inaonyesha kuwa tarehe 07/08/2018, pande zote mbili, mlalamikaji na mlalamikiwa hawakuwepo katika usuluhishi. Tarehe 07/10/2018, mlalamikaji hakuwepo na ndipo mgogoro ukafutwa. Mahakama inaona

Labour Court Tz.

kuwa endapo Msuluhishi angezingatia hoja hizi, angeweza kutoa maamuzi yaliyo sahihi na ya haki kwa pande zote.

Msuluhishi hakujielekeza katika ukweli kuwa hati za wito zilizowasilishwa zilitolewa kabla ya kufutwa kwa mgogoro tarehe 07/10/2018 na haukuwepo ushahidi endapo hati ya wito ilitolewa kwa mleta maombi baada ya shauri kurejeshwa. Hivyo hoja ya tatu inajibiwa kuwa msuluhishi alikosea katika kufanya maamuzi yake. Na kwa hiyo, hoja ya kwanza kuwa endapo Mleta maombi ametoa sababu za msingi za kutengua uamuzi wa upande mmoja nayo inajibiwa kwa kukubaliwa na Mahakama hii kwa kuzingatia sababu nilizofafanua hapo juu, na kwa kuzingatia utoaji haki kwa pande zote, naona kuwa upo umuhimu wa Mleta maombi kupewa nafasi ya kusikilizwa kwa kuzingatia mazingira ya shauri hili kama yaliyofafanuliwa hapo juu na Mahakama hii.

Kwa msingi huu ninakubali maombi haya na kutengua uamuzi na Tuzo ya upande mmoja uliotolewa na Amos. A, Msuluhishi, tarehe 22/02/2019 na pia ninatengua uamuzi mdogo wa maombi ya kutengua uamuzi na Tuzo ya upande mmoja uliotolewa na Kalinga. C, Msuluhishi tarehe 15/10/2019. Ninaamuru kuwa shauri lirejeshwe mbele ya Tume na kusikilizwa upya pande zote mbili. Kila upande utajigharamia gharama zake za kuendesha shauri hili. Haki ya kukata rufaa imeelezwa.

Labour Court TZ.

Imeamriwa.

A. Msafiri.

**JAJI**

05/07/2021

Labour Court Tz.